# JARIDA LA MWEZI

TOLEO NA. 051

MACHI 2025



## 1 TMA YAADHIMISHA SIKU YA HALI YA HEWA DUNIANI KWA KUTOA ELIMU NCHINI

## 2 MRADI WA HUDUMA ZA TAHADHARI ZA HALI MBAYA YA HALI YA HEWA WAZINDULIWA RASMI TANZANIA



## 3 FAHAMU ZAIDI:
## HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI FEBRUARI, 2023



KITAIFA

# TMA YAADHIMISHA SIKU YA HALI YA HEWA DUNIANI KWA KUTOA ELIMU NCHINI

**Dodoma**



Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ilitadhimisha Siku ya Hali ya Hewa Duniani (WMD) Machi 23, 2025 kwa kutoa elimu katika maeneo mbalimbali nchini pamoja na kusheherekea miaka 75 tangu kuanzishwa kwa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO).

Katika siku hiyo, Naibu Waziri wa Uchukuzi Mhe. David Mwakiposa Kihenzile alitoa ujumbe kwa umma akimwakilisha Waziri wa Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa na kupongeza kazi nzuri inayofanywa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kwa kutoa huduma bora.

“Katika Siku hii ya Hali ya Hewa Duniani, Serikali inapongeza kazi nzuri inayofanywa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) katika utoaji wa huduma za hali ya hewa zilizoboreshwa sana, ikiwa ni pamoja na utoaji wa

tahadhari wakati wa matukio ya hali mbaya ya hewa". Alisema Mhe. Kihenzile.



Mhe. Kihenzile alieleza kuwa Serikali itaendelea kuimarisha huduma za hali ya hewa kwa kuwekeza katika miundombinu ya kisasa zaidi na kuendelea kuwajengea uwezo wataalamu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA Dkt. Ladslaus Chang'a alisema Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania imechukua hatua za kimkakati kupitia teknolojia za kisasa kama akili mnemba (AI) kuboresha utabiri na tahadhari za hali mbaya ya hewa.

Kauli mbiu ya mwaka huu ni "Kwa Pamoja Tushughulikie Pengo la Utoaji wa Tahadhari".





KIMATAIFA

# MRADI WA HUDUMA ZA TAHADHARI ZA HALI MBAYA YA HALI YA HEWA WAZINDULIWA RASMI

**Dodoma**




Naibu Waziri wa Wizara ya Uchukuzi, Mhe. David KIhenzile (Mb) akimwakilisha Waziri wa Uchukuzi alizindua rasmi Mradi wa Huduma za Tahadhari za Hali mbaya ya Hewa (Early Warning for All- EW4ALL), Jijini Dodoma, tarehe 19 Machi 2025. Mradi huo unafadhiliwa na nchi ya Denmark ukiwa na lengo la kuhakikisha kuwa kila mtu anafikiwa na huduma za tahadhari hivyo kulindwa dhidi ya matukio ya hali mbaya ya hewa ifikapo mwishoni mwaka 2027.

Katika hotuba yake, Mhe. Kihenzile alisema "Uboreshwaji wa huduma za tahadhari dhidi ya hali mbaya ya hewa ni muhimu sana hasa kwa nchi zinazoendelea, ikiwemo Tanzania, kwani uchumi wa nchi hizi unajengwa zaidi na sekta za kijamii na kiuchumi zinazotegemea sana hali ya hewa, na kwa kuzingatia athari za mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi ambayo yamesababisha matukio ya hali mbaya ya hewa kuwa ya mara kwa mara na ya hatari zaidi, hivyo kuwepo kwa mradi huu ni tija kwa Taifa letu". Alisema Mhe. Kihenzile.

Aidha, Mhe. Kihenzile aliongeza kuwa katika kufikia malengo ya mradi nchini, ushirikiano kati ya washirika wote wanaotekeleza mradi huu unahitajika. "Nitoe rai muendelee kuwa na mtazamo wa pamoja na kuhakikisha kuwa shughuli zinazotekelezwa zinafanyika kwa ufanisi ili kufikia matokeo na malengo yaliyokusudiwa. Ni muhimu kuboresha usambazaji wa taarifa za tahadhari kwa njia zenye tija hasa kwa gharama nafuu ili kuhakikisha kuwa watu wote, wakiwemo wanaoishi maeneo ya vijijini, wanafikiwa na taarifa hizi". Alisisitiza Mhe. Kihenzile.

Mwakilishi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Kanali. Selestine Masalamado

alisema Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu ina jukumu kubwa la kuratibu masuala mbalimbali katika ngazi ya kitaifa ambapo moja ya majukumu yake ni kuratibu hatua za kukabiliana na majanga mbalimbali yakiwemo majanga yatokanayo na matukio ya hali mbaya ya hewa.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na Mwakilishi wa Kudumu wa Shirika la Hali ya Duniani (WMO) na Makamu Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi (IPCC), Dk.Ladislaus Chang'a alisema Ripoti ya Tathmini ya Sita ya Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi (IPCC) imeainisha bayana kuwa matukio ya hali mbaya ya hewa ikiwemo Mvua kubwa, Joto kali, Upepo mkali, Mafuriko, Ukame na Vimbunga yameongezekana yanatarajiwa kuendelea kuongezeka kwa idadi na ukubwa kadri ambavyo joto linaongezeka, na kusababisha majanga makubwa.

Aidha, Dkt. Chang'a aliongezea kuwa "Leo hii tutatoa ripoti yetu ya tathmini ya hali ya Klaimatolojia kwa mwaka 2024 iliyoandaliwa na TMA na pia wasilisho maalaumu litafanywa katika warsha maalumu itakayofanyika leo na kesho sanjali na uzinduzi huu".

Naye Mkurugenzi wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), Dkt. Agnes Kijazi alisema WMO itaendelea kushirikiana na TMA pamoja na wadau wengine katika kuhakikisha lengo linafikiwa na kuhakikisha watanzania wote wanafikiwa na huduma za tahadhari za hali mbaya ya hewa.

Balozi wa Denmark alieleza kuwa Tanzania ni moja kati ya nchi tano za Afrika ambazo zimechaguliwa kutekelza mradi huu kwa ufadhili wa Denmark, na hii ni kutokana na ushirikiano wa muda mrefu uliopo baina ya Tanzania na Denmark katika masuala ya huduma za hali ya hewa.

Mradi huu unatekelezwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kwa kushirikiana na Washirika wengine katika ngazi ya Kitaifa na ya Kimataifa ambao ni Ofisi ya Waziri Mkuu – Idara ya Usimamizi wa Maafa, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kupunguza Hatari za Majanga (UNDRR), Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), Shirika la Mawasiliano la Kimataifa (ITU), Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania (TRCS), na Shirikisho la Kimataifa la Msalaba Mwekundu (IFRC).



# FAHAMU ZAIDI

## HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI APRILI, 2025

Katika kipindi cha mwezi Aprili, 2025 mvua za msimu zinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi nchini. Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa katika baadhi ya maeneo nchini na kusababisha mafuriko, kutuama kwa maji na kuathiri shughuli za kiuchumi. Kwa upande mwingine, hali ya joto inatarajiwa kupungua kidogo, hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua. Aidha katika baadhi ya maeneo yanayotarajiwa kuwa na upungufu wa mvua hali ya joto inatarajiwa kuendelea.

| MAENEO | MAELEZO |
|---|---|
| Pwani ya Kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba): | ♦ Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika maeneo machache katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.** |
| Nyanda za juu Kaskazini Mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara): | ♦ Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa kati ya wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.** |
| Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu): | ♦ Vipindi vya mvua inayoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika maeneo machache katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.** |
| Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): | ♦ Vipindi vya mvua pamoja na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika maeneo machache hususan katika wiki ya kwanza na ya pili.** |
| Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): | ♦ Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika maeneo machache katika wiki ya pili ya mwezi.** |
| Nyanda za juu Kusini Magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro): | ♦ Vipindi vya mvua inayoambatana na ngurumo vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa kati ya wiki ya kwanza na ya pili katika maeneo machache.** |
| Pwani ya Kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): | ♦ Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.** |
| Kanda ya Kusini (Mkoa wa Ruvuma): | ♦ Vipindi vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika wiki ya kwanza ya mwezi.** |


# JE WAJUA?

Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania imefanikisha ununuzi na ufungaji wa rada 5 za hali ya hewa nchini. Rada hizi zilizofungwa katika mikoa mbalimbali nchini kama vile Dar es salaam,Kigoma, Mbeya, Mwanza na Mtwara zina uwezo wa hali ya juu wenye ufanisi wa kuona zaidi ya kilometa za mkato 450 na kuona matone madogo sana ya mvua kwa uhalisia ndani ya kilometa 250. Aidha, rada nyingine mbili zitakazofungwa Kilimanjaro na Dodoma zinaendelewa na utengenezaji.

Uwepo wa rada za hali ya hewa nchini umesaidia upatikanaji wa taarifa sahihi za hali ya hewa na umeimarisha uwezo wa Mamlaka kubaini mapema matukio ya hali mbaya ya hewa na kutoa taarifa sahihi mapema, hivyo kuwezesha Mamlaka zinazohusiana na menejimenti ya maafa kuweza kujiandaa kwa ajili ya kupunguza athari zitokanazo na matukio ya hali mbaya ya hewa ikiwemo kuokoa maisha ya watu na mali zao.








**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA:**

**Mhariri**
Monica Mutoni

**Waandishi**
Monica Mutoni
Kennedy Mgeta

**Msanifu Kurasa**
Kennedy Mgeta

**Shukrani**
Kituo Kikuu cha Utabiri
Kitengo cha Udhibiti na Usimamizi Ubora

www.meteo.go.tz

@tmaservices

@tma_servces

@tanzaniameteorological

www.meteotz1950.blogspot.com

tanzaniametagency

TMAonline TV

Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu,
1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27,
41218 DODOMA.